# HABARI na MATUKIO

Toleo Na. 35 | Tanzania Fertilizer Regulatory Authority | tfra_official | tfra_official | Februari 2026

JARIDA LA KILA MWEZI LA MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA

# SERIKALI NA MIKAKATI KUIMARISHA TASNIA YA MBOLEA NCHINI




Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent, akitoa hotuba katika mkutano wa kimataifa wa wadau wa mbolea Barani Afrika – ARGUS uliofanyika katika hoteli ya Johari Rotana jijini Dar es Salaam Februari 11, 2026.

NDANI>>

WIZARA, TFRA WAPONGEZWA USIMAMIZI MAHIRI TASNIA YA MBOLEA NCHINI 4

WIZARA YA KILIMO ZANZIBAR, TFRA KUIMARISHA USHIRIKIANO WA USIMAMIZI WA MBOLEA 3

# SERIKALI NA MIKAKATI KUIMARISHA TASNIA YA MBOLEA NCHINI

Serikali imesema imejipanga kuhakikisha tasnia ya mbolea nchini inaendelea kuimarika kwa manufaa ya wakulima na maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Hayo yalibainishwa hivi karibuni na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo anayeshughulikia Maendeleo ya Mazao na Usalama wa Chakula, Prof. Peter Msofe, alipozungumza kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Daniel Chongolo, katika mkutano wa kimataifa wa wadau wa mbolea barani Afrika (ARGUS) uliofanyika katika hoteli ya Johari Rotana jijini Dar es Salaam.




Meneja wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja, Elizabeth Bolle (wa kwanza kulia), akizungumza na wawezeshaji walioshiriki wakati wa mkutano wa wadau wa mbolea Barani Afrika – ARGUS uliofanyika katika hoteli ya Johari Rotana jijini Dar es Salaam Februari 11, 2026.

Prof. Msofe alisema serikali inaendelea kuweka mikakati mbalimbali ya kuimarisha upatikanaji na kuongeza matumizi ya mbolea nchini kwani ni nyenzo muhimu ya kimkakati katika kuhakikisha usalama wa chakula, kuongeza uzalishaji wa mazao na kusaidia wakulima kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alifafanua kuwa, Tanzania inaendelea kutekeleza na kuzingatia vipaumbele vya kikanda na Bara Afrika katika maendeleo ya kilimo, ikiwemo kupitia Comprehensive Africa Agriculture Development Programme (CAADP), East African Community (EAC), Southern African Development Community (SADC) na African Continental Free Trade Area (AfCFTA).

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent, alisema Tanzania ni miongoni mwa soko kubwa la mbolea linalokua kwa kasi zaidi barani Afrika.

Alieleza kuwa, matumizi ya mbolea nchini yameongezeka kutoka tani 360,000 mwaka 2021/2022 hadi takribani kufikia tani 972,506 mwaka 2024/2025, huku matarajio yakionyesha mahitaji yataongezeka na kufikia tani milioni 2.1 ifikapo mwaka 2030.

Laurent aliongeza kuwa utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbolea kwa Njia ya Kidijitali umeongeza upatikanaji wa pembejeo hiyo kwa wakulima. Alisema serikali inaendelea kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya kuzalisha mbolea nchini kwa kutumia malighafi zilizopo ndani ya nchi pamoja na kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ubora wa mbolea.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wadau wa tasnia ya mbolea waliohudhuria mkutano huo walisema kuwa wamepata fursa ya kukutana na wadau kutoka nchi mbalimbali na kubadilishana uzoefu kuhusu biashara ya mbolea, jambo litakalosaidia kuchochea ukuaji wa sekta hiyo nchini.



Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi kutoka TFRA, Victoria Elangwa (wa kwanza kulia), akifuatilia mada wakati wa mkutano wa kimataifa wa wadau wa mbolea Barani Afrika – ARGUS uliofanyika katika hoteli ya Johari Rotana jijini Dar es Salaam Februari 11, 2026.

# WIZARA YA KILIMO ZANZIBAR, TFRA KUIMARISHA USHIRIKIANO WA USIMAMIZI WA MBOLEA

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema itaendelea kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania katika kuhakikisha wakulima wanapata mbolea bora ili kuongeza uzalishaji wa mazao na kuchochea maendeleo ya sekta ya kilimo visiwani humo.

Akizungumza wakati wa ziara ya kikazi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) iliyofanyika Februari 2, 2026, Naibu Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Zanzibar, Dkt. Salum Soud Hamed, alisema ushirikiano huo utasaidia kuhakikisha wakulima wanapata pembejeo bora kwa wakati na hivyo kuongeza tija ya uzalishaji na kuboresha maisha yao.

Dkt. Salum alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaona umuhimu wa kuimarisha ushirikiano huo kupitia kuingia Makubaliano ya Kiutendaji (MoU) kati ya Wizara ya Kilimo Zanzibar na TFRA, yatakayosaidia kuboresha na kuimarisha mahusiano ya kiutendaji kwa manufaa ya maendeleo ya sekta ya kilimo na uchumi wa Taifa kwa ujumla.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent (wa kwanza kushoto), akizungumza wakati wa kikao baina ya watendaji wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Zanzibar na wataalam wa TFRA tarehe 2 Februari 2026.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Fertilizer Regulatory Authority, Joel Laurent, alisema ushirikiano wa karibu kati ya TFRA na Wizara ya Kilimo Zanzibar ni muhimu katika kuhakikisha wakulima wanapata mbolea yenye ubora unaokubalika na kwa wakati.

Aliongeza kuwa kubadilishana uzoefu, maarifa na mbinu bora za usimamizi wa pembejeo hiyo baina ya Tanzania Bara na Zanzibar kutasaidia kuimarisha mifumo ya udhibiti wa mbolea, kuongeza ufanisi katika kusimamia tasnia hiyo na kulinda maslahi ya wakulima.

Aidha, alisema hatua hiyo itachangia kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo na kuimarisha usalama wa chakula nchini.

Ziara hiyo ya TFRA katika Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Zanzibar ililenga kubadilishana uzoefu na kujifunza mbinu bora za usimamizi na udhibiti wa mbolea kati ya Tanzania Bara na Zanzibar, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuongeza tija ya uzalishaji wa kilimo na kuboresha maisha ya wakulima.



Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent (watano kulia), Naibu Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Zanzibar, Dkt. Salum Soud Hamed (wanne kulia), pamoja na viongozi na wataalamu wa TFRA na Wizara ya Kilimo Zanzibar wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kikao cha kuimarisha ushirikiano baina ya pande hizo kilichofanyika Zanzibar tarehe 2 Februari 2026.

# WIZARA, TFRA WAPONGEZWA USIMAMIZI MAHIRI TASNIA YA MBOLEA NCHINI

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, Mhe. Deodatus Mwanyika, ameipongeza Wizara ya Kilimo kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yake katika kusimamia tasnia ya mbolea nchini yenye mchango mkubwa katika kukuza sekta ya kilimo na kuchangia ukuaji wa uchumi wa taifa.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Bw. Joel Laurent, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka kwa kipindi cha miaka mitano (2021/22–2025/26), akieleza mafanikio yaliyopatikana na mikakati ya kuimarisha zaidi usimamizi wa tasnia ya mbolea nchini.

Mhe.Mwanyika alitoa pongezi hizo wakati wa kikao cha pamoja baina ya Kamati hiyo, Wizara ya Kilimo na Menejimenti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Kilichofanyika Jijini Dodoma hivi karibuni.

Akizungumza katika Kikao hicho kilicholenga kufuatilia shughuli za usimamizi wa tasnia ya mbolea nchini Mhe. Mwanyika alikuwa alibainisha kuwa mamlaka imekuwa ikifanya kazi nzuri ya kuhakikisha mbolea inapatikana kwa wakati tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Akizungumzia kuhusu zoezi la upimaji wa afya ya udongo wenye lengo la kuwafanya wakulima kutumia mbolea kulingana na mahitaji ya udongo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Bw. Gerald Mweli, alieleza kwamba tayari zoezi limekamilika katika mikoa 19 nchini, na mikoa sita iliyosalia zoezi hilo litakamilika ndani ya kipindi cha miezi mitatu ijayo.

Mweli aliongeza kwamba wizara inaandaa ramani ya afya ya udongo itakayokuwa ikionyesha maeneo yote yaliyopimwa, hatua itakayowasaidia wakulima kutumia mbolea kwa usahihi ili kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao mbalimbali, huku wizara ikiwa imepanga kuanzisha mashamba darasa katika kila kata nchini ili kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea kwa vitendo kwa wakulima.



Mkurugenzi wa Uzalishaji wa ndani na Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja, Louis Kasera (Kushoto) akifuatiwa na Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Happiness Mbelle (Katikati) na Meneja wa Uingizaji na Usafirishaji wa Mbolea, Dotto Deteba, wakati wa kikao cha pamoja baina ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, Wizara ya Kilimo na TFRA.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2021/22 hadi 2025/26, Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent, ameeleza kuwa matokeo mazuri yaliyopatikana pamoja na mikakati ya kuendelea kuimarisha usimamizi na udhibiti wa tasnia ya mbolea nchini umechangiwa na uongozi thabiti wa serikali ya Awamu ya Sita.

Kikao hicho kilikuwa kikiibua majadiliano kuhusu hatua za kuendeleza upatikanaji wa mbolea, ubora wake, na kuimarisha elimu kwa wakulima, huku wajumbe wakitoa mapendekezo ya kuendeleza ushirikiano kati ya wizara, TFRA na wadau wote ili kuhakikisha malengo ya sekta ya kilimo yanatimizwa.

# TFRA, ZALIRI KUIMARISHA USHIRIKIANO KATIKA TAFITI ZA MBOLEA

Ushirikiano kati ya taasisi za udhibiti na utafiti wa kilimo umetajwa kuwa muhimu katika kuhakikisha matumizi ya mbolea yenye ubora na tija kwa wakulima nchini.

Akizungumza Februari 3, 2026 katika ofisi za Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZALIRI), Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti kutoka Tanzania Fertilizer Regulatory Authority (TFRA), Happiness Mbelle, alisema ushirikiano kati ya TFRA na taasisi za utafiti ni muhimu katika kuhakikisha mbolea zenye ubunifu na teknolojia mpya zinafanyiwa tafiti za kisayansi kabla ya kutumika na wakulima.

Alisema tafiti hizo zinahusisha pia mbolea bunifu zinazotengenezwa kwa kutumia malighafi mbalimbali ikiwemo mbolea zinazotokana na zao la mwani, ili kuhakikisha zinakidhi viwango vya ubora vinavyotakiwa na kuchangia kuongeza tija na uzalishaji wa mazao.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Mbelle alisema mamlaka hiyo itaendelea kushirikiana na ZALIRI katika kubadilishana taarifa za kitaalamu, kufanya tafiti shirikishi na kutumia matokeo ya tafiti hizo kuboresha mifumo ya usimamizi na udhibiti wa mbolea nchini.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuhakikisha wakulima wanapata mbolea bora na kutumia pembejeo hizo kwa ufanisi zaidi, jambo litakaloongeza uzalishaji wa mazao na kuchangia usalama wa chakula.

Kwa upande wake, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZALIRI), Masoud Said, alisema taasisi hiyo iko tayari kushirikiana na TFRA katika kuendeleza tafiti zinazolenga kuboresha uzalishaji wa mazao, matumizi sahihi ya mbolea na kulinda afya ya udongo.

Aliongeza kuwa, ushirikiano huo utawezesha matumizi ya sayansi na teknolojia katika sekta ya kilimo, hatua itakayochangia kuongeza uzalishaji wa mazao pamoja na kuimarisha mchango wa kilimo katika uchumi wa Zanzibar na Taifa kwa ujumla.



Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Happiness Mbelle, akizungumza tarehe 3 Februari 2026 katika ofisi za Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZALIRI) wakati wa kikao cha kujadili ushirikiano katika tafiti za ufanisi wa matumizi ya mbolea shambani.

# MBOLEA ZA MWANI ZAFUNGUA FURSA MPYA ZA KILIMO HAI ZANZIBAR NA TANZANIA BARA



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent, akiwa katika kikao kazi na viongozi wa Kampuni ya Mwani Zanzibar (ZASCO) katika Wilaya ya Kaskazini Pemba, Zanzibar, tarehe 4 Februari 2026.

Ujenzi wa kiwanda cha kuchakata mbolea za mwani katika Wilaya ya Kaskazini Pemba unatajwa kuwa hatua muhimu katika kufungua fursa mpya za kilimo hai, kuongeza tija ya mazao ya mbogamboga, matunda na viungo, pamoja na kuimarisha uchumi wa wakulima Zanzibar na Tanzania Bara.

Akizungumza Februari 4, 2026, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent, alisema Zanzibar ina fursa kubwa ya kuendeleza kilimo kutokana na mwelekeo wake wa uzalishaji wa mbogamboga, matunda na viungo.

Laurent alisema, kiwanda cha uchakata mbolea za mwani kitarahisisha upatikanaji wa mbolea bora za kikaboni (organic), kuongeza uzalishaji na kuboresha ubora wa mazao. Aliongeza kuwa, masoko ya mbolea za kikaboni yanakua kwa kasi Tanzania Bara, jambo linaloongeza nafasi ya kibiashara ya mbolea za mwani na kukuza kilimo endelevu.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Mwani Zanzibar (ZASCO), Mwadini Haji, alisema mradi huo unatarajiwa kuzalisha tani 24,000 za mbolea kwa kutumia mwani mkavu na tani 60,000 kwa kutumia mwani mbichi. Hatua hiyo itapanua upatikanaji wa mbolea za kikaboni kwa wakulima na kukuza matumizi ya pembejeo rafiki kwa mazingira.

Haji alisema ZASCO inategemewa kuwa kiunganishi muhimu kwa wakulima kwa kuwapatia mbolea salama na zenye kuongeza ubora wa mazao, sambamba na kuinua thamani ya zao la mwani.

Naye Mkurugenzi wa Masoko wa ZASCO, Kazija Mussa Msheba, alisema baada ya kuanza uzalishaji wa mbolea hizo, kampuni itaanzisha mashamba darasa Zanzibar na Tanzania Bara ili kuwajengea wakulima uelewa wa matumizi sahihi ya mbolea za mwani kwa vitendo na kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao.

# WAKULIMA CHEMBA WATAAKIWA KUJISAJILI ILI KUNUFAIKA NA RUZUKU ZA PEMBEJEO

Wakulima katika Halmashauri ya Wilaya ya Chemba mkoani Dodoma wanatakiwa kujisajili katika mfumo rasmi wa pembejeo za ruzuku ili kunufaika na ruzuku zinazotolewa na serikali kwa wakulima.

Hayo yalibainishwa Februari 16, 2026, na Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Kanda ya Kati, Levocatus Rwegoshora, wakati wa kampeni ya Mali Shambani iliyolenga kuhamasisha wakulima kununua pembejeo kupitia mfumo rasmi na kupata bidhaa zenye ubora kwa bei nafuu.

Rwegoshora alisema usajili huo unawawezesha wakulima kunufaika moja kwa moja na Mpango wa Ruzuku za Pembejeo za Kilimo wa Serikali, jambo litakalosaidia kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao yao.

Akizungumza kwa niaba ya Taasisi ya Kuthibitisha Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), Mtafiti na Mkaguzi wa Ubora wa Mbegu, Dkt. Neema Yohana, alisema serikali inatoa ruzuku ya pembejeo muhimu za kilimo ikiwemo mbegu, mbolea na viuatilifu. Alisisitiza kuwa wakulima wanapaswa kununua pembejeo hizo kupitia mfumo rasmi ili kupata bidhaa zilizoidhinishwa na zenye ubora.

Dkt. Yohana aliongeza kuwa wakulima wanaweza kuthibitisha ubora wa mbegu kwa kutumia vocha zilizopo kwenye kifungashio cha mbegu kwa kupiga 14852# na kufuata maelekezo kisha kuingiza namba ya vocha ili kujiridhisha kama mbegu ni halisi na imeidhinishwa.

Kampeni ya Mali Shambani inalenga pia kuongeza uelewa kwa wakulima kuhusu matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo, umuhimu wa kupima afya ya udongo na kujisajili katika mpango wa ruzuku. Hatua hiyo inatarajiwa kuchochea uzalishaji wenye tija na kuimarisha usalama wa chakula nchini.



Wakulima wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba mkoani Dodoma wakifuatilia mafunzo ya matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo (mbegu, mbolea na viuatilifu) ikiwa ni utekelezaji wa kampeni Mali Shambani, Februari 16, 2026.

# WAKULIMA CHEMBA WATAAKIWA KUJISAJILI ILI KUNUFAIKA NA RUZUKU ZA PEMBEJEO



Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Kanda ya Kati, Levocatus Rwegoshora, akizungumza wakati wa kampeni ya Mali Shambani iliyolenga kuhamasisha wakulima kujisajili katika mfumo rasmi wa ruzuku Februari 16, 2026.



Mkulima wa kijiji cha Paranga, Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, Ramadhani Sunuku, akiushukuru timu ya wataalam kutoka Wizara ya Kilimo kupitia kampeni ya Mali Shambani baada ya kuhamasika kujisajili kwenye mpango wa ruzuku wa pembejeo za kilimo.

# WAKULIMA GAIRO WAFIKIWA NA ELIMU YA MATUMIZI SAHIHI YA PEMBEJEO

Wakulima wa vijiji vya Kibedya na Rubeho katika Wilaya ya Gairo mkoani Morogoro wahimizwa kuzingatia matumizi sahihi ya pembejeo na kupima afya ya udongo ili kuongeza tija, kulinda mazingira na kuinua kipato kupitia kilimo cha kisasa.

Akizungumza Februari 17, 2026, Afisa Kilimo kutoka Wizara ya Kilimo, Alphonce Mwiru, alisema serikali inaendelea na zoezi la upimaji wa udongo kote nchini ili kubaini mahitaji halisi ya virutubisho kwenye mashamba. Aliongeza kuwa hatua hiyo itawawezesha wakulima kutumia mbolea kwa usahihi kulingana na aina ya udongo wa shamba.



Afisa Kilimo wa Kijiji cha Kibedya, Rahim Hamis, alisema wameanzisha mashamba darasa kwa lengo la kuwafundisha wakulima kwa vitendo mbinu bora za kilimo, hatua inayotarajiwa kuongeza uzalishaji wa mazao katika Wilaya ya Gairo, Februari 17, 2026.



Afisa Udhibiti Ubora kutoka TFRA, John Wambura, akizungumza na wakulima katika Kijiji cha Rubeho, Wilaya ya Gairo mkoani Morogoro, Februari 17, 2026, ambapo alisisitiza kuwa mafanikio ya matumizi ya pembejeo yanategemea upimaji wa afya ya udongo na kuwahimiza wakulima kupima mashamba yao kabla ya kutumia mbolea.

Kwa upande wake, Afisa Udhibiti Ubora kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), John Wambura, alisisitiza kuwa, mafanikio ya matumizi ya pembejeo yanategemea upimaji wa afya ya udongo, na kuwahimiza wakulima kupima mashamba yao kabla ya kutumia mbolea.

Aidha, Afisa Masoko kutoka Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), Is-haq Ibrahim Mwalimu, aliwataka wakulima kujiandikisha kwenye mfumo wa kidijitali wa ruzuku ili kupata mbolea kwa bei himilivu na kwa wakati. Alieleza kuwa mfumo huo unaongeza uwazi na kurahisisha upatikanaji wa pembejeo.

Wakulima Dani Mashasha na Twaha Ramadhani walisema elimu ya matumizi sahihi ya pembejeo imeongeza uelewa na matumaini ya mavuno bora, wakisisitiza umuhimu wa kuachana na kilimo cha mazoea na kuhamia kwenye kilimo cha kisasa chenye tija.

Afisa Kilimo wa Kijiji cha Kibedya, Rahim Hamis, alisema wameanzisha mashamba darasa kwa lengo la kuwafundisha wakulima mbinu bora za kilimo kwa vitendo, hatua inayotarajiwa kuongeza uzalishaji wa mazao katika Wilaya ya Gairo.

# KILIMO CHENYE TIJA HUANZA NA MATUMIZI SAHIHI YA PEMBEJEO



Wakulima wa Skimu ya Umwagiliaji ya Mawala, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, wakifuatilia mafunzo ya matumizi sahihi ya mbolea ikiwa ni utekelezaji wa kampeni Mali Shambani, Februari 20, 2026.

Wakulima katika Skimu ya Umwagiliaji ya Mawala, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, wamehimizwa kuachana na kilimo cha mazoea na kuzingatia matumizi sahihi ya pembejeo ili kuongeza uzalishaji na kipato.

Wito huo umetolewa Februari 19, 2026, wakati wa kampeni ya Mali Shambani inayofanywa na Wizara ya Kilimo na taasisi zake, yenye lengo la kutoa elimu kwa wakulima juu ya matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo.

Akizungumza katika mafunzo hayo, Afisa Kilimo na Mkaguzi wa Maduka ya Pembejeo Moshi DC, Hamza Mwinyihija, alisema mwamko wa wakulima katika kutumia pembejeo sahihi umeongezeka, jambo linaloashiria mabadiliko chanya katika sekta ya kilimo. Alisisitiza kuwa bila matumizi sahihi ya pembejeo, mkulima hawezi kupata matokeo bora, na kuongeza kuwa kilimo katika wilaya hiyo kina historia ndefu hivyo ni muhimu kuendana na mbinu za kisasa ili kuongeza tija.

Kwa upande wake, mkulima wa mpunga katika skimu hiyo, Julitha Fredy, alisema mafunzo kuhusu matumizi sahihi ya mbolea yameongeza ari na matumaini mapya ya kuongeza uzalishaji. Alibainisha kuwa kabla ya elimu hiyo, wakulima wengi walitumia pembejeo bila kufuata kanuni sahihi, jambo lililopunguza mavuno.

Mkulima mwingine, Dismas Shelukindo, alisema mafunzo yaliyotolewa yataongeza tija kwa wakulima, hususan katika matumizi ya mbegu bora na mbolea. Aliongeza kuwa, elimu hiyo imewasaidia kuelewa umuhimu wa kuchagua pembejeo kulingana na mahitaji ya udongo na zao husika.



Mkulima wa mpunga katika Skimu ya Umwagiliaji ya Mawala mkoani Kilimanjaro, Dismas Shelukindo, akizungumza katika mafunzo ya matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo. Alisema mafunzo hayo yataongeza tija kwa wakulima hususan katika matumizi ya mbegu bora na mbolea, na pia yamemsaidia kuelewa umuhimu wa kuchagua pembejeo kulingana na mahitaji ya udongo na zao husika, Februari 20, 2026.

# KILIMO BORA CHACHOCHEA TIJA NA UZALISHAJI KWA WAKULIMA

Wakulima wa Kijiji cha Matui, Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara, wamehimizwa kuzingatia matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo, hususan mbolea, ili kuongeza tija na kuboresha maisha yao kupitia kilimo chenye tija na cha kibiashara.



Wakulima wa Kijiji cha Matui, Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara, wakifuatilia mafunzo ya matumizi sahihi ya mbolea ikiwa ni utekelezaji wa kampeni Mali Shambani, Februari 23, 2026.

Wito huo ulitolewa Februari 23, 2026, ikiwa ni utekelezaji wa kampeni ya Mali Shambani, inayofanywa na Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na taasisi zake, ili kuhamasisha matumizi sahihi ya pembejeo na kuongeza uelewa kwa wakulima kuhusu kanuni bora za kilimo.

Akizungumza katika mafunzo hayo, Afisa Udhibiti Ubora kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Said Sembade, alisema lengo kuu la kampeni hiyo ni kutoa elimu na ushauri wa kitaalamu kuhusu matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo pamoja na kuhamasisha wakulima kuzitumia kwa kuzingatia kanuni bora. Alisisitiza kuwa matumizi sahihi ya mbolea huanza na upimaji wa afya ya udongo ili kubaini mahitaji halisi ya virutubisho kabla ya kununua na kutumia.

Aidha, alisema TFRA inaendelea kuhamasisha wakulima kujisajili katika mpango wa ruzuku ya mbolea na kushirikiana kwa karibu na maafisa ugani wa vijiji na kata ili kuhakikisha wakulima wanapata elimu sahihi kuhusu umuhimu wa mbolea katika kuongeza uzalishaji.




Afisa Udhibiti Ubora kutoka TFRA, Said Sembade, akizungumza kuhusu lengo kuu la kampeni ya Mali Shambani, ya kutoa elimu na ushauri wa kitaalamu kuhusu matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo, alipokuwa katika Kijiji cha Matui, Februari 23, 2026.

Kwa upande wake, mkulima wa kijiji hicho, Zubeda Bakari Kalanga, alisema mafunzo hayo yamebadili mtazamo wake kuhusu matumizi ya mbolea. Awali aliamini mbolea za viwandani huharibu udongo, lakini sasa ameelewa kuwa matumizi yasiyo sahihi ndiyo husababisha madhara.

Aliongeza kuwa tofauti ya mavuno ni kubwa kati ya mkulima anayetumia pembejeo sahihi na asiyetumia, akibainisha kuwa licha ya kulima eneo dogo, mavuno yake yameongezeka kutokana na matumizi sahihi ya mbegu bora, mbolea na viuatilifu.

Uhamasishaji huo unaendelea kuwa chachu ya mabadiliko chanya katika uzalishaji na maendeleo katika sekta ya kilimo.

# USAJILI WA WAKULIMA KIDIJITALI WAIMARISHA UPATIKANAJI WA MBOLEA YA RUZUKU

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) imesisitiza umuhimu wa wakulima kujisajili katika mfumo wa kidijitali ili kuwezesha upatikanaji wa pembejeo, hususan kupitia mpango wa ruzuku wa Serikali unaolenga kuongeza tija ya uzalishaji wa mavuno.

Akizungumza Februari 23, 2026, katika vijiji vya Kwamsisi na Kwasunga, wilayani Handeni mkoani Tanga, Afisa Udhibiti Ubora kutoka TFRA, Peter Mwanguku, alisema usajili wa kidijitali wa mfumo wa pembejeo unasaidia kubaini mahitaji halisi ya pembejeo kwa kila eneo nchini.

Kwa upande wake, Afisa Kilimo kutoka Wizara ya Kilimo, Alphonce Mwiru, alisema mfumo wa kidijitali umeongeza uwazi na ufanisi kwa kuwawezesha maafisa kilimo na wasimamizi wa pembejeo kufuatilia takwimu za wakulima, aina ya mazao wanayolima na mahitaji yao kwa misimu husika.

Naye mkulima, Athumani Ibrahim Hassan, kutoka kijiji cha Kwasunga, alishukuru Serikali kwa kuendelea kuboresha elimu ya matumizi sahihi ya pembejeo na kusema hatua hiyo itawawezesha wakulima kupata mavuno mengi na kuongeza kipato cha familia zao.

TFRA kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Halmashauri inaendelea kutoa elimu na kuhamasisha wakulima kujisajili mapema ili kuhakikisha wananufaika kikamilifu na mpango wa ruzuku wa pembejeo.



Afisa Udhibiti Ubora kutoka TFRA, Peter Mwanguku, akitoa elimu kuhusu matumizi sahihi ya pembejeo kwa wakulima katika Kijiji cha Kwamsisi, Wilaya ya Handeni mkoani Tanga, Februari 23, 2026.



Wananchi wa kijiji cha Kwamsisi, Wilaya ya Handeni mkoani Tanga, wakifuatilia mafunzo ya matumizi sahihi ya pembejeo kutoka kwa wataalam wa Wizara ya Kilimo na taasisi zake, Februari 23, 2026.

# VIJANA WATAKIWA KUCHANGAMKIA FURSA KATIKA KILIMO

Vijana wa Wilaya ya Hanang, mkoani Manyara, wanatakiwa kuchangamkia fursa za kilimo cha kibiashara kwa kuzingatia matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo ili kuongeza tija na kipato.

Wito huo umetolewa Februari 24, 2026, katika mwendelezo wa kampeni ya Mali Shambani, inayotekelezwa na Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na taasisi zake ikiwemo Tanzania Fertilizer Regulatory Authority (TFRA).

Akizungumza wakati wa tukio hilo, Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Manyara anayesimamia Sekta ya Uchumi na Uzalishaji, Faraja Ngerageza, alisema taifa linategemea kilimo kama uti wa mgongo wa uchumi na chanzo cha kulifanya taifa kuwa ghala la chakula Afrika. Aliongeza kuwa hakuna kilimo chenye tija bila matumizi sahihi ya pembejeo, na kuwaalika vijana kutumia fursa zilizopo ikiwemo ruzuku ya mbolea na huduma za upimaji afya ya udongo.

Mkuu wa Wilaya ya Hanang, Mhe. Almishi Hazali, alisema zaidi ya asilimia 90 ya mapato ya halmashauri yanatokana na kilimo. Aliongeza kuwa mazingira wezeshi yaliyowekwa na Serikali ya awamu ya sita, ikiwemo ruzuku ya pembejeo na elimu ya matumizi sahihi ya pembejeo, yamepa nafasi vijana kuingia katika kilimo cha biashara. “Hata mimi ni mkulima wa kibiashara; kilimo kina faida na kinahamasisha vijana kujiajiri,” alisisitiza.

Naye mkulima wa mahindi katika kijiji cha Masakta, Salome Msuya, aliwahimiza vijana kujiingiza katika kilimo kwa kuwa sasa ni biashara yenye tija na mafanikio yanayoonekana.

Kilimo kinaendelea kuwa mhimili muhimu wa kuinua uchumi wa vijana na jamii kwa ujumla, hasa pale kinapofanywa kwa kuzingatia kanuni bora na matumizi sahihi ya pembejeo.



Mtafiti na Mkaguzi Ubora wa Mbegu kutoka Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), Dkt. Neema Yohana, akiwaeleza wakulima wa Kijiji cha Nar, Halmashauri ya Wilaya Babati mkoani Manyara jinsi ya kufanya zoezi la T-Hakiki ili kuhakiki ubora wa mbegu, tarehe 25 Februari 2026.

# VIJANA WATAKIWA KUCHANGAMKIA FURSA KATIKA KILIMO



Wakulima 472 wa Kijiji cha Masakta, Halmashauri ya Wilaya ya Hanang mkoani Manyara, wakifuatilia mafunzo ya matumizi sahihi ya mbolea ikiwa ni utekelezaji wa kampeni Mali Shambani, Februari 24, 2026.



Wakulima wa Kijiji cha Gusse, Halmashauri ya Wilaya ya Babati, wakifuatilia mafunzo ya matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo ikiwa ni muendelezo wa kampeni ya Mali Shambani, tarehe 25 Februari 2026.

# TFRA YAENDELEA KUIMARISHA USHIRIKIANO NA WAZALISHAJI WA NDANI WA MBOLEA

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) ilimtembelea mkulima anayelima mbogamboga katika Mtaa wa Mpiji Muheza, Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani, kwa lengo la kujionea ufanisi wa mbolea iliyozalishwa na kijana wa Kitanzania ya Mtetezi Halisi.

Akizungumza shambani hapo tarehe 28 Februari,2026 afisa udhibiti ubora mwandamizi kutoka TFRA Stephano Mfugale alisema kuwa ziara hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya taasisi, kuhakikisha kuwa uzalishaji wa ndani wa mbolea na visaidizi vyake unaongezeka.

Mfugale aliongeza kuwa TFRA inaendelea kuzitangaza fursa za uwekezaji katika tasnia ya mbolea na kuwapongeza wazalishaji wa Mtetezi Halisi kwa kuchangamkia fursa hiyo.



Afisa Udhibiti Ubora Mwandamizi kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Stephano Mfugale (Kushoto), akizungumza na Mkurugenzi wa kampuni ya Mtetezi Halisi inayozalisha mbolea za kimiminika, Raymond Simya, katika Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani, wakati wa ziara ya ukaguzi na kujionea uzalishaji wa mbolea za ndani.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa kampuni ya Mtetezi Halisi inayozalisha mbolea za kimiminika Raymond Simya, alishukuru TFRA kwa ushirikiano walioupata hadi kufanikisha usajili wa mbolea hiyo.



Afisa Udhibiti Ubora Mwandamizi kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Stephano Mfugale, akizungumza na mkulima wa mbogamboga katika Wilaya ya Kibaha, mkoani Pwani, wakati wa ziara ya kukagua na kutoa elimu kuhusu matumizi sahihi ya mbolea ili kuongeza tija katika uzalishaji.

Simya alisema, hatua hiyo imefungua fursa kwa wazalishaji wa ndani kushiriki kikamilifu katika tasnia ya mbolea.

Kwa upande wake, mkulima anayetumia mbolea za Mtetezi Halisi Rehema Bombo alisema tangu aanze kutumia mbolea hiyo ameshuhudia mabadiliko chanya katika ukuaji wa mazao yake.

TFRA inatekeleza majukumu yake kwa kuwafikia wadau wakiwemo wazalishaji wa ndani wa mbolea na wafanyabiashara na wakulima ili kuhakikisha tasnia ya mbolea inaimarika zaidi.